



BARAZA LA DIASPORA LA WATANZANIA DUNIANI

Kumb. TDC20220202/01

TANGAZO KWA WANACHAMA-TDC GLOBAL NA UMMA
MKUTANO MKUU NA UCHAGUZI 2022

Baraza la Diaspora Watanzania Duniani -TDC Global linawatangazia Wanachama na Umma kuwa, Mkutano Mkuu na uchaguzi wa viongozi uliokuwa unatarajiwa kufanyika tarehe 21 hadi 23 Julai 2022 jijini Dodoma Tanzania umebadilishwa. Badala yake Mkutano huo utafanyika kwa njia ya mtandao tarehe 23 Julai 2022.

Taratibu za kushiriki Mkutano Mkuu na uchaguzi wa Viongozi wa TDC Global kupitia mtandao, zitatolewa kwa kadri zinavyokamilika. Uongozi unawakumbusha wanachama kulipia Ada zao, ili wakidhi vigezo vya kikatiba vya kuchagua na kuchaguliwa kupitia mkutano huo.

Kubadilishwa kwa mkutano huo kumetokana kuingiliana na ratiba ya Kongamano la Diaspora linalotarajiwa kufanyika nchini Tanzania, na kusimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uongozi unaomba radhi kwa usumbufu wowote utakao jitokeza kutokana na mabadiliko hayo.

Kwa mawasiliano, maoni au ushauri kuhusu Mkutano Mkuu wa TDC Global tafadhali wasiliana nasi kupitia kupitia barua pepe: maoni@tdcglobal.org

TDC Global inatoa shukrani za dhati kwa wanachama na umma kwa ushirikiano mnaotupatia.

Asanteni sana.

“Diaspora na Nyumbani“

Bkyettiti

Bupe Amon Kyelu

Mwenyekiti

TDC Global

2022-02-02

